# HII NDIYO SIKU ALIYO IFANYA BWANA

Zaburi 117, 1 na 4, 16ab-17, 22-23

Siku ya Mungu ya Paska (Ufufuko wa Bwana)

Musique: Innocent BISHIKWABO




1. Mshukuruni Bwana kwani ndiye mwema,
   Kwani wema wake ndio wa milele.
   Wenye kumwabudu Bwana waseme:
   Kweli wema wake ndio wa milele.

2. Mkono wa kuume wa Bwana umetukuzwa,
   Mkono wa Bwana wa kuume umetenda makubwa.
   Sitakufa, lakini nitaishi,
   Tena nitahubiri matendo ya Bwana.

3. Jiwe walilokataa wajengaji,
   Hilo limekuwa jiwe la pembe:
   Ndilo jambo alilofanya Bwana,
   Nasi twaliona ajabu.

Sikukuu njema ya Paska kwa wote (Bukavu 2025)